Mut'a Ndoa Sahihi

Author(s):

Omar Jumaa Mayunga [3]

Hii Kitabu imeandikwa kwakuelemisha kuhusu Ndoa ya Mu'taa kama ndoa sahihi.
Nakuelezea kutoka Msahafu na Hadithi.

Category:

General [4]
Marriage [5]

Topic Tags:

Mut'a (Temporary marriage) [6]

Miscellaneous information:
Mut'a Ndoa Sahihi Kimeandikwa na Omar Jumaa Mayunga Kimechapishwa na S.L.P. 70005 Dar es Salaam – Tanzania

Featured Category:

Shi'a beliefs explained [7]

Alhamdulillahi, kila sifa njema ni ya Mwenyeezi Mngu, Bwana wa walimwengu. Na Rehma na Amani zimshukie Bwana wetu na Muombezi wetu Muhammad S.A.W., na ziwashukie Aali zake watakatifu, na wanaofuata na kuusimamia uongozi wao mpaka siku ya mwisho.

Ndoa ya Mut'a ni katika mas'ala waliyokhitilafiana Shia na Sunni kutoka mwishomwisho wa utawala wa Khalifa wa pili (Umar bunul Khattab) mpaka leo. Tarehe 17/8/1988 kwa tarehe 3 Muharram 1408 katika ukumbi wa Bilal house, Mombasa, nilizungumza juu ya ndoa ya Mut'a.

Tarehe 1/9/1989 katika Msikiti wa Al'azhar Mombasa, Sheikh Muhammad Sharif Famau alinijibu. Sheikh alizungumzia mambo matano:–

a) Uadilifu wa Masahaba.

b) Tahriful Quran.

c) Wilayatu Ali A.S.

d) Taqiyya.

e) Ndoa ya Mut'a.

Mimi katika kitabu hiki nitashughulika na Mut'a, na haya mengine yameshaanza kujibiwa na Mzee wangu Sheikh Abdilahi Nassir. Kwa hivyo, yeyote anayependa kujua majibu ya vifungu hivyo atasoma vitabu vya Sheikh Abdilahi vya majibu hayo.

a) Sheikh Muhammad Sharif katika darsa yake alizungumzia kwamba:-

b) Mut'a ilikuwako wakati wa Mtume.

c) Kisha Mtume aliiondoa kabla ya yeye kufa.

Kwa hivyo hivi sasa Mut'a ni haramu yeyote anayeoa hivyo ANAZINI.

Kwa mtazamo wa Sheikh Muhammad Sharif Mut'a ni Zina, na ametoa hoja zake.

Kwa hakika, nachukua nafasi hii kumpa pongezi za kweli kabisa. Ndugu yangu Sheikh Muhammad Sharif Famau kwa hatua aliyochukua ya kusahihisha lile ambalo anaona linapotoshwa nje ya misingi ya Islam. Huu ndio msimamo wa Islam, na mwislamu anapaswa kuwa hivi.

Sisi tuko tayari kujadili Qadhia ya Mut'a kwa ukamilifu, lakini kwa sharti:

a) Hatutaki matukano wala kejeli.

b) Tuzungumze kielimu.

Kwa hivyo sisi tunaonyesha:-

a) Mut'a ilikuwako wakati wa Mtume,

b) Mtume S.A.W. hakuiondoa mpaka amekufa.

c) Kwa hivyo ndoa hii si haramu, ni halali mpaka siku ya mwisho.

Kuthibitisha hayo, kutalazimu kuvunja hoja za Sheikh Muhammad Sharif, na kutoa dalili za kuthibitisha kuwa iko, kutokana na vitabu vinavyokubaliwa na Sunni wote.

Mwenyeezi Mngu atupe TAWFIQ, Ee Mola! Tuonyeshe Haki tuifahamu kuwa ni Haki uturuzuku kuifuata. Na tuonyeshe batili tuifahamu kuwa ni batili uturuzuku kuiepuka.

Omar Jumaa Mayunga
24/1/1410

24/10/1989

Kwanza kabla ya yote lazima tujue Mut'a ni nini.

Sheikh Muhammad Sharif ameeleza hivi "Nikaha ya Mut'a ni:Mtu kukutana na mwanamke akamwambia: Mama! hebu nikuoe kiasi cha dakika kumi". Amuoe kwa dakika kumi, akisha ampe kama ni shilingi kumi an shilingi tano, khalas! mambo yamekwisha. Hiyo ndiyo nikaha ya mut'a, haina haja ya shahidi, haina haja ya Walii, hakuna habari ya chakula, hakuna kurithiana, na muda ukisha, khalas, hakuna nikaha tena mpaka uongezwe (baada ya kuieleza hivyo, akasema) Sallaaaaa La! Si upuuzi huo. (watu wakacheka) Mwisho wa kunukuu.

Sasa, tuyajadili maneno hayo:

A) Sheikh Muhammad kwanini hakutoa taarifa ya Mut'a ya ki Istilahi? Kwa faida ya wasomaji wetu, hapa tutatoa taarifa ya Mut'a:-

Mut'a ni: "Kukuoza mwanamke nafsi yake kwa kutaja mahari, na kwa muda maalumu".

B) Sheikh baada ya kutoa taarifa yake akasema:-

Sallaaaala! Si upuuzi huo, yaani Ndoa ya Mut'a ni upuuzi! TUNAULIZA:- Ikiwa anakubali ilikuwako kwa Mtume S.A.W. hiyo ni upunzi? Mtume S.A.W. anafanya upuuzi? Au wakati huo ilikuwa na Shahidi? au Waili? au mirathi? au chakula?

C) Pengine Sheikh anaona ajabu vipi mke wa Mut'a atakuwa Zawj hali ndoa yake haina: Shahidi, Walii, Chakula, mirathi. Hilo lisimshtue! Hata kwa ndoa ya daima huwezekana hilo.

Walii

Amesema Abu Hanifa na Zufar na Sha'aby na Zuhry:

"Atakapofunga ndoa mwanamke bila ya walii na akawa mume huyo ni kuf'u (anayefanana naye kwa akhlaq) ndoa hiyo ni sahihi".

TAZ: Bidayatul Mujtahid J. 2 uk. 10 Mughni ya Ibnu Quddama J. 7 uk. 337.

Shahidi

Amesema Ibn Mundhir:- "Haikuthibiti habari yoyote (sahihi) katika kushuhudia ndoa." Na hivi ndivyo walivyokuwa wakifanya (kuoa bila ya kuweka mashahidi) Abdullah bin Umar (mtoto wa Khalifa wa pili) na Alhasan bin Ali, Ibnuz Zubeir, Salim, na Hamza (watoto wa Ibnu Umar).

Taz

Mughni ya Ibnu Quddama J. 7 uk. 339

Nailul Awtar J. 6 uk. 260

Fiqhus Sunna J. 2 uk. 57

Bidayatul Mujtahid J. 2 uk. 19

Ikhtilaful Ulamaa uk. 123

Chakula

Amesema Muhammad Abdul Rahmani:- "Mwanamke Nashiz (anaegoma kuingiliwa na mumewe) ni haramu kwa Ijmai, kunaondoa haki ya kupewa chakula".

TAZ: Rahmatul Umma fyi Ikhtilafil aimma uk. 224.

Imepokewa kutoka kwa Nakh'i na Sha'aby wamesema:

"Chakula ni mukabala wa jimai (kumwingilia) atakapozuia kuingiliwa, atazuiliwa kupewa chakula".

TAZ: Fiqhus Sunna J. 2 uk. 151 na 149

a) Mwanamke Ahlulkitabi aliyeolewa na Mwislamu, hawezi kumrithi mumewe.

TAZ: Bidayatul Mujtahid J. 2 uk. 381 Sublus salam J. 3 uk. 954

b) Mwanamke aliyemuua mumewe. Amesema Mtume S.A.W. "Muuwaji hana kitu."

TAZ: Fiqhus Sunna J. 3 uk. 427.

Kwa hiyo majibu yetu hapa ni:-

Ndoa ya Mut'a inatimia bila ya Waiji, wala shahidi, wala chakula, wala kurithiana.

Zaidi ya hayo, tunayaona ya Umar bunul Khattab:- Imepokewa kwa:- Abu Salamata bin Sufyani kuwa:- Mwanamke mmoja alikuja kwa Umar bunul Khattab akamwambia:- "Ewe Amierul Muuminina! Nilikwenda kwenye soko la mbuzi wangu, akanikuta mtu mmoja. Akanikusanyia mafungu matatu ya tende, kisha amenichukua. Umar akamuuliza, unasemaje? Yule mwanamke akarudia kama alivyosema kwanza. Umar akamwambia, (hayo ni) Mahari, mahari, mahari, kisha akamwacha (akaenda zake).

TAZ: AL'MUHALLA J.11 uk. 250.

Je! Palikuwa na walii hapo?

Palikuwa na Shahidi?

Sheikh Muhammad vilevile amesema:- "Sisi hatusemi kwamba mut'a haikuwako katika Uislamu, mut'a ilikuwako: Wahaswalatil mut'a fyi dhurufin qasin (Imepatikana mut'a katika mazingira magumu) Wakati wana shida, masahaba wametoka wamekwenda vitani, wameketi muda mrefu, wenda mshitakia Mtume Alaa Nastakhswi Ya Rasulallah? (Je! tujivunje maume?) Shida! Waenda kwa Mtume S.A.W. kwamba afadhali tujikhasi. Mtume S.A.W. akawaambia:- La, la, la, la, ila hilo! haiwezekani! Wakapatiwa nafasi ya mut'a kwa dharura. Wakati wa vita nje ya Mji! Hawako Mjini kwao." Mwisho wa kunukuu.

TUNAULIZA:- Je! Dharura hiyo sasa haipatikani? Watu hawasafiri nje ya miji yao?

Masheikh wa kisunii wanakubali kuwa: Dharura hiyo iko, isipokuwa hawapendelei kuiondoa kwa Mut'a badala yake baadhi yao wanapendelea Ponyeto (kujipuli) maana yake kuchezea utupu kwa mkono au na kitu kingine kwa kuwezesha kutoa manii. Wengine wanapendelea Khadaa. Baadhi ya masheikh wa Kihanafi na baadhi ya masheikh wa Kihanbali.

Taz

Sublus Salami J. 3 uk. 974

Fiqhus Sunna J. 2 uk. 368

Alhalalu Walharamu uk. 161

Kwa upande wa pili wa wanaopendelea Khadaa:-

Amesema Ahmad bin Taymiyya:- "Mtu akisafiri nje ya Mji wake

(basi anayo haki ya) kuoa, atatia nia moyoni mwake kuwa, 'Ninamuoa mwanamke huyu kwa muda fulani, na nikisha rejea Mjini kwangu nitamwacha.'"

TAZ: Fatawa ya Ahmad bin Taymiyya J. 32 uk. 147.

Maana yake, Mwanamke aliyeolewa kwa ndoa namna hii yeye huwa hajui kuwa ufikapo muda fulani (alionuia mume) ataachika. Bali yeye mwanamke analolijua ni kwamba: Ameolewa na wataishi na mumewe daima!! Kumbe amehadaiwa!!! Je! lipi bora:-

Mut'a au kupoteza watoto kwa kujipuli?

Mut'a au kumhadaa mwanamke na ukawa utamwacha ghafla?

Khulasa

a) Mut'a ilikuwako wakati wa Mtume.

b) Ndoa hiyo si upuuzi, hasha Mtume S.A.W. kuruhusu upuuzi.

c) Si kosa kuwa haina shahid, Walii, chakula wala kurithi.

d) Hata ndoa za daima, kwa Sunni huwa hivyo.

e) Dharura iliyowekewa Mut'a mpaka leo iko, kwa hivyo lazima iendelee.

f) Baadhi ya masheikh wa kisunni wanakubali kuwa dharura iko, lakini wao wanapendelea kujipuli na kuhadaa. LIPI BORA!!

1. Ndoa ya Mut'a na ya daima, hazithibiti ila kwa kufungamana na matamko mawili: IJABUN na QABUL (Nimekuoza, Nimekubali).

2. Kufungamana kwa ndoa mbili hizi hakupatikani ila kwa moja kati ya matamko matatu haya: ZAWWAJ'TUKA, ANKAH'TU KA, MATTA'ATUKA.

3. Ndoa mbili hizi hupatisha haramu kwa: Nasabu, Ukwe, Kunyonya.

4. Mtoto wa Mut'a ni kama mtoto wa ndoa ya daima, anazo haki zote.

5. Mke atakaa eda baada ya kumalizika muda wake katika ndoa ya Mut'a, (atakaa eda hedhi mbili, ikiwa mwanamke hapati hedhi basi atakaa siku arobaini na tano) kama ambavyo atakaa eda baada ya kuachika mke wa ndoa ya daima. Itakapokuwa wawili hawa walikwisha ingiliwa.

6. Hakuna eda kwa mwanamke ambae hakuingiliwa, iwe ni ndoa ya daima au ndoa ya Mut'a.

7. Haijuzu kumuoa Shangazi ya mke wa Mut'a (binti ya kaka yake, au binti ya dada yake) ila kwa idhini ya mkeo.

8. Haifai kabisa kumwingilia mke wa Mut'a akiwa katika hali ya siku zake za hedhi au nifasi. Kama ambavyo inakatazwa kwa mke wa daima.

9. Kile kitendo cha kumwingilia mke wa Mut'a kinatoa haki kwa mtoto kuwa ni wa mume huyu, hata kama maji yake (manii) alimwagia nje. Ndivyo ilivyo pia katika ndoa ya daima.

10. Mahari katika ndoa ya Mut'a ni kama katika ndoa ya daima, hakuna kiwango maalum, iwe kidogo sana au nyingi sana. Soma Quran 4:20.

11. Haifai kwa mwanamke wa Kiislamu kuolewa Mut'a na kafiri, kama ambavyo mwanamume haifai kumuoa mwanamke kafiri isipokuwa Ahlulkitabi.

12. Ikigundulika aibu yoyote inayotengua ndoa, basi palepale ndoa huvunjika. Ikiwa alikuwa hajamwingilia basi hana mahari, na kama alikwisha kumwingilia, na mwanamke hakujua kutoka mwanzo aibu hiyo, basi atapewa mahari yote waliyokubaliana. Ikiwa wakati wakifunga ndoa mwanamke alijua hili la kuvunja ndoa akalificha, basi huyo ni malaya hana mahari.

13. Mke wa ndoa ya daima na wa ndoa ya Mut'a, wanapaswa kukaa eda mara mume wao anapokufa, kwa muda wa miezi minne na siku kumi.

14. Eda ya mwenye mimba ni kuzaa mimba yake, iwe ni mke wa daima au wa mut'a.

15. Mume wa ndoa ya Mut'a ana haki ya kumwachia muda wote waliokubaliana kuowana, na kuanzia hapo atakuwa si mkewe tena. Kama ambavyo, mume wa ndoa ya daima anayo haki ya kumpa talaka mkewe.

16. Mume wa ndoa ya Mut'a akimwachia mkewe muda wote waliokubaliana kuowana kabla ya kumwingilia, itapasa ampe nusu ya mahari. Ikiwa walikaa na mke huyo muda wote uliotajwa katika ndoa yao, ukamalizika bila va kumwingilia, itapasa ampe mahari yote.

17. Mume na mke waliowana kwa Mut'a wana haki ya kuongeza muda zaidi kabla ya kumalizika wa kwanza.

Sasa tumwangalie Sheikh Muhammad Sharif Famau, yeye anasema: Kuna kauli mbili kuhusu Mut'a:-

1. Jamhurus sahaba wanaharamisha. Hii ni kauli ya Ali bin Abi Talib, Umar bunul Khattab, Ibnu Masuud, Ibnu Umar, Ibnuz Zubeir, Maimamu wanne, na mattabii wengi.

Kisha akasema:- Kwa Sayyidna Ali peke yake kuharamisha Mut'a kumepokewa Hadithi thamanta a'shara (kumi na nane).

2. Kuwa Mut'a inafaa, Hii ni kauli ya Ibnu Abbas, Ubayya bin Kaab, A'taa, Jabir bin Abdiliah, Abu Said Alkhudury.

1. Ni wazi hili ni jambo Mukhtalafun fihi kwa hiyo halina Ijamaus Sahaba, basi, huweza kuliharamisha.

2. Kwa nini hakuzitaja hizo riwaya kumi na nane za Imam Ali ili tuzijibu?!

3. Sisi tunasema:- Siyo kweli kuhusu Imam Ali, kama tutakavyoonyesha katika kitabu hiki, na hapo atakapozitaja riwaya nyingine.

Sasa, tutazichambua hoja zake, moja moja, nazo ni hizi:-

1. Imepokewa kwa Ibnu Shihab, kutoka kwa Abdullahi na Alhasan, watoto wa Muhammad bin Ali, kutoka kwa baba yao, kutoka kwa Ali bin Abi Talib A.S. kwamba: Mtume S.A.W. amekataza ndoa ya Mut'a siku ya Khaybara na amekataza kula nyama ya punda wa mjini."

2. Imepokewa na Umar bin Alharith na Allaith bin Saad, kwamba Rabi'i bin Sabura Al'jahniyamewasimulia kutoka kwa baba yao, kwamba: Mtume S.A.W. amekataza ndoa ya Mut'a mwaka wa Fat'hu."

3. Imepokewa kwa Abdul Azizi bin Umar bin Abdul Azizi kutoka kwa mtu mmoja wa Sabrini (Rabi'i bin Sabura) kutoka kwa baba yake kuwa yeye amesema. Nimemsikia Mtume S.A.W. anasema katika Hija ya mwisho: Hakika Mwenyeezi Mngu ameharamisha ndoa ya Mut'a, basi msiikaribie na yeyote aliye naye (mke wa Mut'a) na amwache."

4. Amesema Ismail kutoka kwa Az'Zuhry. Tulikuwa kwa Umar bin Abdul'Azizi tukajikumbusha Mut'a, mtu mmoja aitwaye Ar'Rabii bin Saburaakasema:- Nashuhudia kuwa baba yangu amesema kwamba: Mtume S.A.W. amekataza ndoa hiyo katika Hija ya mwisho.

5. Imepokewa kwa Sufyani bin Uyayna kutoka kwa Az'Zuhry' kutoka kwa Ar'Rabii bin Sabura kutoka kwa baba yake kwamba: Mtume S.A.W. amekataza ndoa ya Mut'a mwaka wa Fat'hu Makka.

Hizo ndizo hadithi alizotutajia Sheikh Muhammad Sharif Famau, kisha akasema: "Hizi ni hadithi ambazo zaonyesha kuwa ndoa ya Mut'a ni haramu."

Majibu Yetu

Tunasema:- Kama hizo ndizo hadithi alizozitegemea Sheikh basi ametegemea kamba mbovu. Kama tutakavyoona hivi sasa inshaallah.

1) Hadithi ya Imam Ali A.S. siku ya Khaybara, haikubaliani na tukio la tarikh siku hiyo, kama walivyosema wazi haya wanazuom wengi wa kisunni.

Amesema Ibnu Qayyim Al'jawaziyya:- Kisa cha Khaybara, hakuna sahaba aliyeowa Mut'a mwanamke wa kiyahudi mahala hapo. Wala Mtume S.A.W. hakutoa ruhusa ya jambo hilo, wala hakuna yeyote aliyepokea (habari hizi kwa usahihi) katika vita vya Khaybara na wala hapakuwa pakitajwa Mut'a mahala hapo, si kwa kufanya Mut'a wala kuharamisha Mut'a."

TAZ: Zadul Maad J. 2 uk. 143.

Anaendelea kutusimulia Ibnu Qayyim:- "Kwa hakika Khaybara hapakuwako wanawake wa kiislamu, bali walikuwako tu wanawake wa kiyahudi. Na ruhusa ya kuowa Ahlul kitabi ilikuwa haijatolewa bado, kwa sababu ruhusa hiyo imekuja bada ya tukio ya Khaybara.

TAZ: Fat'hul Bari J. 7 uk.483

Fat'hul Bari J. 9 uk. 168

2) Ikiwa ni hivyo, Imam Ali A.S. hawezi kuwa mjinga hivyo wa kutojua aliyoyajua Ibnu Qayyim na Ibnu Hajar.

3) Lililothibiti kwa Imam Ali A.S. katika vitabu vyetu vya kishia nikwamba:- "Alikuwa akihalalisha". Na katika vitabu vya kisunni nikwamba: "Alikuwa akilaumu Umar bunul Khattab kuiharamisha".

TAZ: Tafsirul Tabari J. 5 uk. 9

Kwa hiyo, hadithi hiyo imeanguka!! Katika hadithi tano ailizotuletea zimebaki hadithi nne.

Alipotoa hadithi hizo alijuwa zina Idhtirab, mara:

Siku ya Khaybara, mara hija ya mwisho, mara Fat'hu Makka.

Sheikh Muhammad Sharif Famau alijitetea kwa mfano wa mtu anaemdai shilingi elfu moja, kuna mashahidi watatu:-

Shahidi wa kwanza anasema:- "Aliona nikimkopesha shilingi elfu moja mwaka 1981.

Shahidi wa pili anasema:- "Aliona nikimkopesha shilingi elfu moja mwaka 1982.

Shahidi wa tatu anasema:- "Aliona nikimkopesha shilingi elfu moja mwaka 1983.

Sheikh Muhammad akauliza:- Muhimu n, HAL THABATAT TAHRIM AM LAM YATH'BUT? Maana yake Je! Umethibiti uharamu au haukuthibiti?

Mifano aliyotoa haiwezi kukubalika katika mahakama yoyote adilifu. Mashahidi watatu wataje miaka mitatu tofauti ya kitendo kimoja?!

Ieleweke kuwa hapo inayohusika si miaka (wakati) peke yake, na mahala vilevile.

Tazama imetajwa, Khaybara na Makka Je! Mashahidi wako wakisema: Waliona ukimkopesha Mombasa shilingi elfu moja, wapili Dar es Salaam, watatu Kampala. Bado hapana Idhtirab??

Je ikiwa hiyo miaka mitatu yote ilitolewa na mtu moja, akasema: Aliona ukimkopesha mtu huyo mmoja mwaka 1981 Mombasa, mwaka 1982 Dar es Salaam, mwaka 1983 Kampala, bado haidhuru Idhtirab?/ Hivi ndivyo zilivyo hadithi nne zilizobaki, zote zimepokewa kwa mtu mmoja Ar'Rabii bin Sabura Al'Jahny.

Zaidi ya hvyo, mtu huyohuyo mmoja riwaya zake zina Idhtirab. Sheikh Muhammad Sharif anatuambia

kuwa:- "Idhtirab hii ingekuwa mbaya, lau kama mtu angesema: Mtume S.A.W. ameharamisha Mut'a mwaka wa Khaybara, ikaja riwaya ya pili kasema: Mtume S.A.W. amehalalisha Mut'a mwaka ya Khaybara idhtirab ndiyo ingedhuru. Lakini hii haidhuru, hukumu ni ileile moja." Mwisho wa kunukuu.

Majibu Yetu

Anasema Ar'Rabii bin Sabura (kama ilivyo katika Sahihi Muslimu na Musnad Ahmad) ruhusa (ya Mut'a) ilikuwa baada ya siku kumi na tano kuingia Makka.

Anasema tena Ar'Rabii bin Sabura:- (kama ilivyo katika Sahihi Muslim na Musnad Ahmad) ruhusa (ya Mut'a) ilikuwa wakati wa kuingia Makka, (anasema) wakati tulipofika Makka, tukatufu, kisha tukaamrishwa kuowa Mut'a. Bila shaka Sheikh amefahamikiwa kuwa Idhtirab hii imedhuru.

Muenyeezi Mngu amesaema: "Mnaostarehe nao katika wao, (Wanawake) basi wapeni mahari yao yaliolazimishwa" 4:24. Aya hii imeshuka katika ndoa ya Mut'a kama ilivyo atika Tafsiri zifuatazo:-

1. Tafsirut Tabari J. 2 uk. 9

2. Addurrul Manthur J. 2 uk. 140

3. Tafsir Ibnu Kathir J. 1 uk. 486

4. Mukhtasar Tafsir Ibnu Kathir J. 1 uk. 375

5. Tafsirul Qurtubi J. 5 uk. 130

6. Tafsirui Khazin J. 1 uk. 506

7. Tafsirul Kash'shaf J. 1 uk. 519

8. Tafsirul Kabir J. 3 uk. 200

9. Tafsirul Maraghi J. 5 uk. 8

10. Tafsirul Alus J. 5 uk. 5

11. Tafsir Abi Hayyan J. 3 uk. 218

12. Tafsir Mujahid uk. 152

13. Ahkamul Quran, Alqadh Abubakar 1/162

14. Ahkamul Quran, Aljassas J. 2 uk. 147

Hata Sheikh Muhammad Sharif naye anakubali, yeye anasema:-

"Kwa ufupi, nikaha ya Mut'a Aya iambiwayo kwamba ndiyo dalili ya nikaha ya Mut'a, japo wanazuoni wengi wa Ahlus Sunna wanasema:- "Famastamta'atum bihi minhunna faatuuhunna ujuura hunna" kwamba hii Aya ilikuja katika nikaha ya Mut'a, Aya hii haihusiani na nikaha ya Mut'a aslani". Mwisho wa kunukuu.

Kwa mujibu wa kauli yake Sheikh, wanazuoni wengi wa Ahlus Sunna wanasema Aya ilikuja katika ndoa ya Mut'a. Lakini yeye hakubali!! Amuweni nyinyi wasomaji wetu.

Mpenzi msomaji, tafadliali sikiliza kaseti zangu nilizozunguinza juu ya Mut'a tarehe 17-8-1988, kisha usikilize kaseti alizonijibu Sheikh Muhammad Sharif Famau tarehe 1-9-1989. Baada ya hapo jibu letu hili ulisome kwa makini na mazingatio yenye ikhlas ya kutafuta haki. Nataraji jibu la mushkeli huu utalipata inshaalla.

Imepokewa kwa Jaabir Bin Abdullah Al'Ansar amesema:-

"Sisi tulikuwa tukifanya Mut'a wakati wa Mtume S.A.W. na wakati wa Abubakar na nusu katika utawala wa Umar, kisha akaikataza Umar."

TAZAMA:

- Fat'hul Bari J. 11 uk. 76
- Umdatul Qary J. 8 uk. 310
- Sharhu Sahihi Muslim J. 8 uk. 233
- Musnadu Ahmad J. 3 uk. 380
- Bidayatul Mujtahid J. 2 uk. 58
- Zadul Maad J. 1 uk. 208 - 209.

Sheikh Muhammad Sharif yeye anasema"ILIKUWAKO" si sawa na "IKO MPAKA LEO" Basi jambo gani lililofanya Shia waamini iko mpaka leo? Ni sababu nne:

1. Ni mutawatir katika vitabu vyetu vya hadithi, hilo peke yake linatosha.

2. Haijathibiti kuwa imenasikhiwa, hata kwa hadithi za Sunni kama tulivyoona katika masomo yaliyopita.

3. Lililothibiti ni kuwa iliendelea baada ya Mtume S.A.W. kufariki.

4. Sayydna Umar ndiye aliyeiondoa na yeye hana uwezo huo. Ushahidi, aliyeiondoa ni Umar:- Amesema Umar bunul Khattab:- "Mut'a mbili zilikuwako wakati wa Mtume, na mimi nazikataza na natoa adhabu (kwa atakefanya) Tamauuu ya Hija na ndoa ya Mut'a.

TAZAMA:

Tafsirul Kabir 3.3 uk. 200

Musnad Ahmad J.1 uk. 52

Al'Mughuniya ya Ibnu Quddama J. 7 uk. 572

Sheikh Muhammad Sharif anashangaa, vipi sahaba walimwogopa Umar, wakanyamaza wasimpinge?

Jawabu:- Hakuogopewa. Wako waliompinga kwa vitendo, wakaendelea kuoa na kuolewa Mut'a bila kujali maneno yake. Katika waliompinga Umar ni:-

1. Imam Ali bin Talib A.S.

2. Abdullah bin Abbas A.S.

3. Imran bin Alhuswain Alkhuzai A.S.

4. Jaabir bin Abdullah Al'Ansar A.S.

5. Abdullahi bin Masuud. A.S.

6. Abu Said Alkhudry A.S.

7. Said bin Jubair A.S.

8. Abdallah bin Umar.

9. Rabia bin Ummi bin Kaab Al'Ansar.

10. Az'Zubeir bin Al'Awwam Al'qurash.

11. Salmata bin Umayya Al'jamhi.

12. Maabad bin Umayya Al'jamhi.

13. Muawia bin Abu Sufyan.

Haya utayapata katika vitabu hivi:-

1. Tafsirut Tabari J. 5 uk. 9

2. Bidayatul Mujtahid J. 2 uk. 63

3. Lisanul Arab J. 14 uk. 66

4. Taajul A'rus J. 10 uk. 200

5. Al'Faiq ya Az'Zamakhshary J. 1 uk. 331

6. Al'Muhalla J. 9 uk. 519

7. Sharhu Sahihi Muslim J.11 uk. 186

Kama ambavyo masunni wote wamempuuza Umar bunul Khattab, katika Tamattu'u ya Hija wanaendelea bila kujali kelele zake. Tazama vitabu vyao (Masunni) vya Fiq'h katika mlango:- AINA ZA KUHIRIMIA wamegawanya aina tatu:- QIRAN, TAMATU'U, (ambayo Umar bunul Khattab ameipiga marfuku) na IFRAD. Wanazuoni wote wa kisunni wamekubaliana waendelee nazo, licha ya kukataza Umar Tamattu'u ya Hija.

TAZAMA: Fiq'hus Sunna J.1 uk. 553

Na hata kama walinyamaza, ni aibu? Kwani hawakunyamaza?

Alipoonya kwamba Mtume hakufa? "Imesimuliwa na mwana Aisha kuwa:- Zilipotangazwa habari za kifo cha Mtume S.A.W. Umar bunul Khattab na Mughira bin Shuuba waliomba kuingia chumbani alikolazwa Mtume S.A.W. walipoingia, wakamfunua uso, Umar akasema: Oh msiba nizito! Kuondokewa Mtume S.A.W. kisha wa-katoka walipofika mlangoni, Mughira akasema: "Ewe Umar! Kwa kweli Mtume amekufa." Umar akajibu: "Wewe muongo, Mtume hajafa, isipokuwa wewe muongo, ni mtu unayesumbuliwa na fitina, mtume S.A.W. hatakufa mpaka wanafiki wamalizike wote."

TAZAMA: Albidayatu Wannihaya J.5 uk. 212 Umar akaanza kuonya kuwa:- Nitakae nisikia anasema Mtume amekufa nitakata kichwa chake, wako wanafiki wanadai kuwa Miume amekufa, na wala hakufa. Umar hakunyamaza mpaka alipomuona Abubakar kafika akakaa chini!!!

Alipofanya talaka tatu ni tatu? Imepokewa kwa Abdillahi bin Ali bin Assaib, kutoka kwa Nafii bin Ajiiz bin Abdi Yazid kwamba: "Rukana bin Abdi Yazid alimpa talaka tatu mkewe, Mtume akapewa habari hiyo, akaamuru mke arejeshwe kwa mumewe mara moja.

TAZAMA: Tafsirul Qurtubi J .3 uk. 131

Fiq'hus Sunna J. 2 uk. 231

Kwa hiyo katika zama za Mtume S.A.W. mtu akiacha talaka tatu mara moja huhesabiwa ni talaka moja tu, kwa mujibu wa hukumu ya Mtume S.A.W. Mwenyeezi Mngu anasema:- "Haiwi wa mwanamume aliyeamini wala mwanamke aliyeamini, Mwenyeezi Mngu na Mtume wake wanapokata shauri, wawe na

hiari katika shauri lao." 33:36. Ulipofika utawala wa Umar bunul Khattab yeye akaamuru talaka tatu ni tatu kinyume na amri ya Mtume!!

Alipoleta jamaa ya taraweh?

Mtume hakuleta sala ya taraweh iia wala haikuwako katika zama za Abu Bakar. Katika sala za jamaa za sunna alizofundisha Mtukufu Mtume S.A.W. taraweh haimo, bali huo ni uzushi wa Umar bunul Khattab.

TAZAMA: Al'Kamil fit Tarekh J. 3 uk. 31

At'Tabaqatul Kubra J. 3 uk. 281

Al'Milal Wannihal J. 1 uk. 78

Sheikh Muhammad Sharif anakataa kuwa Umar ndiye aliyekataza Mut'a yeye anasema:-

Ilivyo ni kwamba: Sayyidna Umar alipanda katika mimbari akasema:- "Kwa nini watu wanaowa hii Mut'a na hali Mtume amaeikataza; sikilizeni mimi sitaletewa yeyote aliyeowa ndoa hiyo isipokuwa nitampopoa mawe." Hivyo ndivyo anavyosema Sheikh Muhammad Sharif.

Jawabu:- Hilo halikubaliki, kwa sababu mategemeo ya hadithi hiyo ni mabovu kabisa.

TAZAMA: A'jarhu Wattaa'adil J. 4 uk. 171

Mizanul Itidali J. 4 uk. 184

Lisanul Mizani J. 6 uk. 95

Sasa, vipi utalinganisha hadithi hiyo na zile tulizokwisha zitaja?!!. Kwa hiyo riwaya hiyo haina mashiko tupa nje. Sasa, tuje kwa Ibnu Abbas:- Sheikh Muhammad amesema hivi:- Ibnu Abbas mwenyewe alipokwenda akaulizwa na masahaba kwamba: Ewe Ibnu Abbas Fat'wa yako imefika mbali, watu wametunga mashairi, akasema:- "LA ILAHA ILLALLAH, ASTAGH'FIRULLA INNAMA HIYA KAL'MAYTAT" Hivyo ndiyo alivyosema Sheikh Muhammad, na sisi tunamwambia kuwa maneno ya Ibnu Abbas yalikuwa hivi:- INNA LILLAHI WAINNA ILAYHI RAJIUN WALLAHI MA BIHADHA AFTAYTU WALA HADHA ARADTU WALA AH'LALTU MIN'HA ILLA MA AHALLALLAHU MINAL MAYTATI WADDAMI WALAHMIL KHINZIR".

Maana yake, "Sisi ni wa Mwenyeezi Mngu na sisi tutarejea kwake, Wallahi haya sikuyatolea fat'wa na wala sikuyataka. Na sikuihalalisha ila vile alivyohalalisha Mwenyeezi Mngu katika nyamafu na damu na nyama ya nguruwe."

TAZAMA: Majmauz' Zawaid J. 4 uk. 268.

1. Riwaya hiyo ni ya Said bin Jubeir, ambae alikuwa akifanya Mut'a Makka na Ibnu Abbas pamoja na wafuasi wake walikuwa wakiiona Mut'a kuwani halali.

TAZAMA: Al'Musannaf J. 7 uk. 496

Tafsirul Qurtubi J.5 uk. 133

Al'Mughuniya Ibnu Quddama J. 7 uk. 571

2. Riwaya hiyo ni nyonge sana.

TAZAMA: Tahdhibut Tahdhibi J. 2 uk. 198.

3. Riwaya hiyo ndani yake mna Hajjaji bin Artat:-

"Amesema Ibnu Abdil Hakami, nimemsikia Shafii akisema:

Amesema: Hajjaji bin Artat, Hautimii muruwa wa mtu (heshima) mpaka awache sala ya jamaa nikamwambia, Mwenyeezi Mngu na auondoe murua huu." Amesema Al'Asmai:- Mtu wa kwanza kupokea rushwa Basra katika ukadhini Hajjaji bin Artat."

TAZAMA: Mizanul Itidali J. 1 uk. 459

Sasa, tuache hadithi zilizothibiti, tushike ya mtu, Ambae anaona ni murua kuacha sala ya jamaa? Mtu ambae ndiye kadhi wa kwanza kula rushwa Basra? Hadithi hiyo haina mashiko tupa nje. La ajabu zaidi hapa ni kwamba, japo baadhi ya Masheikh wao wanaharamisha ndoa ya Mut'a, lakini wanaruhusu kujipuli!! Na baadhi ya masheikh wao wamejawizisha Hadaa, kumuowa mwanamke ukinuia utamwacha baada ya muda fulani kufika bila ya yeye kujua!! Fat'wa hii ni ya Ibnu Taymiyya.

TAZAMA: Majmu'u Fatawa Ibnu Taymiyya J.32/147.

Fat'wa ya kujipuli, angalia vitabu:- Alhalalu Walharamu uk. 161

Sublus Sallami J. 3 uk. 974.

Na vingine vingi katika wanazuoni wa Kihanafi na Hanbali waweza kuyapata hayo ya kujawizisha Ponyeto (Kujipuli)

Wanasema:- "Aya isemayo: Na ambao kwa tupu zao ni wenye kujilinda, isipokuwa kwa wake zao au kwa (wanawake) wale iliyowamiliki mikono yao ya kuume, basi hakika hao ndio wasiolaumiwa. Lakini anaetaka kinyume cha haya basi hao ndio warukao mipaka" 23: 5-7. Aya hizi zimeiondoa Mut'a. Jawabu: Aya hizi haziwezi kuiondoa ndoa ya Mut'a kwa sababu, Aya hizi zimeshuka Makka, na Aya ya Muta imeshuka Madina. Kwa mujibu wa misingi va Nasikh na Mansukh dai hili limeanguka, litupe nje.

Wanasema:– "Aya isemayo: Na nyinyi (wanaume) mtapata nusu ya (mali) walizoacha wake zenu" 4:12 inaonyesha kwamba:

Mume atamrithi mke na mke atamrithi mume, jambo ambalo halipatikani kabisa kwenye ndoa va Mut'a.

Jawabu:– Kukosa kurithiana baina ya mume na mke si jambo linaloweza kuzuia kuthibiti ndoa. Bali ndoa inasihi bila ya kuweko kurithiana.

TAZAMA:

Bidayatul Mujtahid J. 2 uk. 381

Sublus Salami J.3 uk. 954

Fiq'hus Sunna J.3 uk. 427

Wanasema:– "Aya isemayo: Ewe Mtume! mnapowaacha wanawake, waacheni katika wakati wa eda zao" 65:1 Aya hii inataja hukumu za talaka kumwacha mwanamke wakati wa eda yake ni kumwacha wakati yuko katika tohara, hana hedhi ambayo hukumwingilia.

Lakini kwa ndoa ya Mut'a hulipati hili, muda ukimalizika waliokubaliana basi, mwanamke anakwenda zake bila ya talaka wala habari ya kukaa eda hakuna.

Jawabu: Zifuatazo ni hukumu za ndoa ya Mut'a, kama ilivyothibiti kwa mujibu wa Sharia:–

1) Ijabu na Qabul:

Mwanamke atasema nimekuoza nafsi yangu kwa muda fulani kwa mahari kiasi fulani. Mume aseme nimekubali.

2) Kutajwa Mahari:

Ni lazima katika ndoa ya Mut'a kitajwe kiwango cha mahari walichokubaliana. Na isipotaiwa ndoa haisihi.

3) Kutajwa Muda:

Katika ndoa ya Mut'a lazima utajwe muda wa kuowana vinginevyo ndoa haitasihi.

4) Mashahidi:

Ndoa ya Mut'a haina haja ya walii wala shahidi.

5) Haifai kuoa Mut'a mwanamke kafiri wala mwanamke malaya.

6) Inafaa kuoa Mut'a mwanamke Ahlul kitabi na Majusi.

7) Mwanamke Bikra:

Hapa wamekhtilafiana, wako waliosema kuwa, mwanamke bikra anaweza kuolewa Mut'a bila ya idhini ya walii wake. Na wako waliosema: Mwanamke bikra lazima asimamiwe na walii wake iwe ni ndoa ya Mut'a au ya daima. Na hii ndiyo Fat'wa ya Asayyid Abdul'qasim Al'musawy Al,khui.

8) Masharti:

Mume na mke wana haki ya kuwekeana sharti, kwa mfano, mume hataki wazae na mkewe muda huu. Au mume na mke wamekubaliana kuwa watarithiana pindi mmoja wao atafariki.

9) Mtoto wa Mut'a:

Mtoto anaezaliwa katika ndoa ya Mut'a ana haki zote sawa na mtoto wa ndoa ya daima.

10) Eda:

Mke wa ndoa ya Mut'a hana talaka, umalizikapo muda waliokubaliana kuoana basi ndoa hukatika. Na kuanzia hapo atakaa eda kwa muda wa hedhi mbili, ikiwa ni mwanamke asiyepata hedhi, basi atakaa eda siku arobaini na tano.

11) Idadi ya Wake:

Inajuzu katika ndoa ya Mut'a kuoa wake wengi, kwa sababu wake wa Mut'a hawaingii katika idadi ya wake wa ndoa ya daima. Kwa hivyo unaweza kuoa wake alfu moja wa Mut'a. Amesema Shafii kuwa:- "Ibnu Jurayhi aliowa Mut'a wake tisini."

TAZAMA:

Tahdhibut Tahdhibi J. 6 uk. 406

Mizanul Itidal J. 2 uk. 151

Tarehe 18/9/1989, katika majira ya saa moja kasorobo asubuhi. Sauti ya Ujerumani ilitangaza kuwa "Katika nchi ya Morocco, ndoa ya Mut'a imeshika nguvu sana. Vijana wa kiume na wakike wanaowana Mut'a kwa idadi kubwa, na inasemekana kuwa Masaudi wengi wanakwenda Morocco kwa ajill ya kuowa Mut'a. Mwanamke wa Morocco hujulikana kuwa ameolewa Mut'a kwa kuonekana mapambo ya dhahabu aliyonayo ambayo huyapata kwa Masaudi."

Basi tunataraji nchi nyingine zitachukua mfano wa Morocco kwa kuimarisha ndoa ya Mut'a. Lakini jukumu hili zaidi linawakabili Waislamu wake kwa waume popote walipo kuisoma na kuitumia ndoa hii, kwa sababu ni Sharia ya Mwenyeezi Mngu na Mtume wake.

Mwenyeezi Mngu anasema:- Haiwi kwa mwanamume aliyeamini wala kwa mwanamke aliyeamini, Mwenyeezi Mngu na Mtume wake wanapokata shauri, wawe na khiyari katika shauri lao. Na mwenye kumuasi Mwenyeezi Mungu na Mtume wake, hakika amepotea upotovu uliowazi." 33:36.

Source URL: https://www.al-islam.org/node/41707

Links

[1] https://www.al-islam.org/user/login?destination=node/41707%23comment-form

[2] https://www.al-islam.org/user/register?destination=node/41707%23comment-form

[3] https://www.al-islam.org/person/omar-jumaa-mayunga

[4] https://www.al-islam.org/library/general-laws-worship

[5] https://www.al-islam.org/library/marriage

[6] https://www.al-islam.org/tags/muta-temporary-marriage

[7] https://www.al-islam.org/feature/shia-beliefs-explained